

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU

11 JUNI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU – TAREHE 11 JUNI, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

355. MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI
(MCHINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwamba Serikali ni pamoja na Serikali za Mitaa na Mtu yoyote anayetokeleza madaraka au mamlaka kwa niaba ya Serikali au Halmashauri:-

Je, kwa nini katika kipindi chote cha uwepo wa Katiba hiyo Serikali haijatunga Sera ya Ugatuuji Madaraka ambayo ingewezesha kuweka mfumo wa Kisheria unaoelekeza mipaka, majukumu na

utaratibu wa utekelezaji wa matakwa hayo ya Kikatiba.

356. MHESHIMIWA JORAM ISMAEL HONGOLI (LUPEMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata yamekuwa ni chanzo cha migogoro badala ya kutatua migogoro:-

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kutoa mafunzo ya muda mfupi ili waweze kumudu majukumu yao kwa ufanisi.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

357. MHESHIMIWA MAHMOUD HASSAN MGIMWA (MUFINDI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Mtiri – Ifwagi – Mdaburo – Ihamu – Mpangataza hadi Mlimba inaunganisha Wilaya ya Mufindi na Kilombero; na ni muhimu sana kiuchumi na kijamii kwa Mikoa hiyo miwili. Aidha, Mheshimiwa Rais aliahidi kuipandisha hadhi barabara hii kuwa chini ya TANROADS:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi barabara hiyo ili kuwa chini ya TANROADS;

(b) Je, kuna mkakati gani wa dharura kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa wakati wote.

358. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Madaraja ya barabara ya Gairo – Chakwale – Idilo – Kilindi yatajengwa au kukarabatiwa ili barabara hiyo iweze kupitika wakati wote wa masika na kiangazi bila matatizo.

WIZARA YA MAJI:

359. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mradi wa Maji wa Mto Mbwinji upo kwenye chanzo chenye maji ya kutosha, ambapo bomba kubwa la maji linaloelekea Nachingwea limepita kwenye Vijiji vyenye matatizo makubwa ya maji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba la maji vinapata huduma hiyo;

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwahakikishia Wananchi wa Ndanda kuwa Zahanati na

Vituo vya Afya vitaunganishwa na huduma hii muhimu ya upatikanaji wa maji.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

360. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Kiwanda cha Tumbaku cha SONAMCU kilichopo Songea Mjini;
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha Kiwanda cha usindikaji wa Samaki wanaotoka Ziwa Nyasa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

361. MHESHIMIWA RUKIA KASSIM AHMED (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Baadhi ya Magereza nchini yamejaa Wafungwa na Mahabusu ambao ni Wakimbizi:-

Je, ni lini Serikali itawarejesha Wakimbizi hao makwao ili kupunguza msongomano ndani ya Magereza yetu.

362. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wilaya ya Tanganyika haina jengo la Polisi Makao Makuu ya Wilaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi eneo la Makao Makuu ya Wilaya.

363. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Eneo la Rubwera Kata ya Kyerwa ndio Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengi yalikuwa ya Wananchi; kuna eneo lilichukuliwa na Jeshi la Magereza na Wananchi walizuiliwa kufanya shughuli yoyote kwenye eneo hilo:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi hawa kama walivyoahidiwa.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:**

**364. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka kipimo
cha MRI katika Hospitali za Amana, Temeke na
Mwananyamala.

**DODOMA
11 JUNI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**